**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

**06** **URAIA NA MAADILI**

**Muda: Saa 1:30** **SULUHISHO** **Mwaka: 2018**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu mbili; A na B zenye jumla ya maswali **sita (06)**
2. Jibu maswali **yote**



Pata hii, pamoja na vitu vingine katika: https://maktaba.tetea.org

*Imeandaliwa na Maria Marco kwa TETEA*

## SEHEMU A (Alama 26)

1. Jibu vipengele (i) – (v) kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuandika katika kisanduku.

(i) Ipi kati ya tabia zifuatazo inaleta uharibifu wa mazingira?
A. Matumizi ya mbolea ya samadi
B. Kumwagilia bustani maji
C. Kukata miti ovyo
D. Kufyeka nyasi
**Jibu: C. Kukata miti ovyo**
Sababu: Kukata miti bila mpango kunasababisha uharibifu wa mazingira na upungufu wa miti.

(ii) Ni faida gani inatokana na matumizi ya chandarua wakati wa kulala?
A. Kuzuia ugonjwa wa kifua kikuu
B. Kuzuia ugonjwa wa malaria
C. Kuzuia ugonjwa wa kipindupindu
D. Kuzuia baridi wakati wa usiku
**Jibu: B. Kuzuia ugonjwa wa malaria**
Sababu: Chandarua huzuia kuumwa na mbu wanaobeba malaria.

(iii) Kitendo cha baadhi ya watoto kuzurura mitaani ni kiashiria cha
A. Tabia ya unafiki
B. Tabia ya majungu
C. Tabia ya tamaa
D. Tabia hatarishi
**Jibu: D. Tabia hatarishi**
Sababu: Kuzurura mitaani kunawaweka watoto kwenye hatari za ajali na uhalifu.

(iv) Ni kwa nini watoto wanashauriwa kukataa kupokea fedha au zawadi kutoka kwa watu wasiowajua?
A. Kuzuia utajiri
B. Kuzuia uzururaji
C. Kuepuka vishawishi


Pata hii, pamoja na vitu vingine katika: https://maktaba.tetea.org
*Imeandaliwa na Maria Marco kwa TETEA*

D. Kuepuka uvivu
**Jibu: C. Kuepuka vishawishi**
Sababu: Kupokea zawadi kutoka kwa watu wasiojulikana kunaweza kuwavua usalama watoto.

2. Jibu kipengele (i) - (iv) kwa kuoanisha majukumu yaliyoainishwa katika Fungu A na vyeo vya wahusika wa majukumu hayo katika Fungu B.

(i) Husimamia mahudhurio na taaluma darasani pamoja na nidhamu.
**Jibu: B. Mwalimu wa darasa**

(ii) Hupanga na kusimamia mipango yote ya maendeleo katika shule.
**Jibu: D. Mwalimu mkuu**

(iii) Husimamia mahudhurio ya wanafunzi shuleni na kuhakikisha kuwa wamevaa sare za shule.
**Jibu: F. Kiranja mkuu**

(iv) Husimamia shughuli zote za uendeshaji wa shule za kila siku.
**Jibu: D. Mwalimu mkuu**

3. Chagua jibu sahihi kutoka kwenye mabano na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi.

(i) Kitendo cha kumwambia mtu alichokifanya sio sahihi ni
**Jibu: kumkosoa**

(ii) Kufanya kazi kwa pamoja inamaanisha
**Jibu: kushirikiana**

(iii) Kufanya mambo mazuri uliyojipangia ni
**Jibu: nidhamu binafsi**

(iv) Nini hutumika kudhibiti tabia za wanafunzi shuleni?
**Jibu: sheria za shule**

**SEHEMU B (Alama 24)**

4. Jibu vipengele (i) – (v) kwa kuonesha matendo yanayoonesha haki au wajibu kwa kuweka alama ya (√) kwenye sehemu inayohusika.


Pata hii, pamoja na vitu vingine katika: https://maktaba.tetea.org
*Imeandaliwa na Maria Marco kwa TETEA*

(ii) Kucheza michezo mbalimbali
**Jibu: Haki √**

(iii) Kuwasaidia wakubwa na wadogo zako
**Jibu: Wajibu √**

(iv) Kupendwa na kupewa mahitaji ya msingi
**Jibu: Haki √**

(v) Kufanya kazi za shule
**Jibu: Wajibu √**

5. Chunguza picha na kisha jibu maswali yanayofuata.

(i) Watu wanaoonekana katika picha wanafanya tendo gani?
**Jibu:** Wanacheza dansi

(ii) Ni kifaa gani cha muziki kinachoonekana kwenye picha?
**Jibu:** Ngoma

(iii) Kitendo cha Wazungu kushirikiana na Waafrika kinaonyesha nini?
**Jibu:** Ushirikiano wa kitamaduni na umoja

(iv) Nini umuhimu wa kujifunza kitendo kinachoonekana kwenye picha?
**Jibu:** Kinafundisha kuheshimu tamaduni nyingine na kukuza mshikamano wa kijamii

6. Soma kifungu cha habari kisha jibu maswali.

Soma kwa makini kifungu cha habari kisha jibu maswali yatakayofuata. Amina ni mwanafunzi wa Darasa la Nne katika shule ya msingi Kibo. Amina anaishi na shangazi yake ambaye ni tajiri sana. Siku zote Amina huenda shuleni bila kula chochote asubuhi wala kupewa kitu cha kula wakati wa mapumziko kwa sababu ya uchoyo wa shangazi yake. Siku moja rafiki yake aitwaye Joani alimshawishi ili amwibie fedha shangazi yake. Amina alikataa na kumwambia rafiki yake kuwa kuiba sio njia ya kutatua matatizo yake. Amina aliendelea kusema, "Naamini iko siku moja nitafanikiwa kwa kufanya bidii katika masomo yangu na shughuli nyingine, halafu nitajitegemea na kuwasaidia wengine.

(i) Shangazi yake Amina ana tabia gani?
**Jibu:** Uchoyo


Pata hii, pamoja na vitu vingine katika: https://maktaba.tetea.org
***Imeandaliwa na Maria Marco kwa TETEA***

(ii) Kwa nini Joani hakuwa rafiki mzuri?
**Jibu:** Alimshawishi Amina kufanya jambo lisilo sahihi, yaani kuiba

(iii) Nani alikuwa na mtazamo chanya kati ya Amina na Joani?
**Jibu:** Amina

(iv) Nani mwenye tabia inayofaa kuigwa kati ya shangazi, Amina na Joani? Toa sababu moja
**Jibu:** Amina, kwa sababu aliweka heshima na nidhamu binafsi na hakufuata njia ya kuiba.


Pata hii, pamoja na vitu vingine katika: https://maktaba.tetea.org
***Imeandaliwa na Maria Marco kwa TETEA***